



*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*

# NAFSI YA MWANADAMU--2

Katika somo letu lililopita tulijifunza ukweli kuhusu "nafsi" na "roho" katika Biblia. Leo tutachunguza baadhi ya maandiko yanayoonekana kupingana kuhusu nafsi. Kuna maeneo machache ambayo yanaonekana kuashiria kwamba nafsi inaendelea kuishi baada ya kifo, jambo ambalo tunajua si kweli.

**Mfalme Sauli na Mchawi wa Endori**

Katika 1 Samweli 28:7-19 Mfalme Sauli wa Israel alimwendea mwanamke mwaguzi (au mchawi) kwa kuwa alitaka kuwasiliana na nabii Samweli aliyekuwa amekufa: "*Ndipo Sauli akawaambia watumishi wake, Nitafutieni mwanamke ambaye ni mwaguzi; ili niende kuuliza kwake. Watumishi wake wakamwambia, tazama, yupo mmoja huko Endori. Basi Sauli akajigeuza, na kuvaa mavazi mengine, kisha akaenda, yeye na watu wawili pamoja naye, wakamfikilia yule mwanamke usiku; akasema, Tafadhali unibashirie kwa utambuzi, ukanipandishie yeye nitakayemtaja kwako.*" (1 Samweli 28:7,8[1]). Mfalme alijua kwamba alipaswa kujificha kwa sababu alitambulika sana katika Israel (taz. 1 Samweli 10:23). "*Lakini yule mwanamke akamwambia, Hakika wewe unajua alichokifanya Sauli,*

[1] Nukuu zote za Maandiko zimetoka katika *Toleo Jipya la* Biblia la Kimataifa isipokuwa kama imetambulishwa vinginevyo.

*Amewakatilia mbali waaguzi, wapiga ramli wote na wachawi kutoka katika nchi. Mbona umenitegea maisha yangu upate kuniua?"* (aya ya 9).

Sheria ya Israel ilikuwa wazi kabisa kuhusu kuwafukuza waaguzi kutoka katika nchi: "*Asipatikane mtu miongoni mwenu....... ambaye ni mchawi, wala mwaguzi, wala mtu alogaye kwa kupiga mafundo, wala mtu awaombaye wafu. Mtu ye yote afanyaye mambo hayo ni chukizo kwa BWANA*" (Kumbukumbu la Torati 18:10-12). Mungu alihesabu kuwa ni chukizo kwa mtu yeyote kutafuta ushauri kwa mlozi, mchawi, au mwaguzi, na Mfalme Sauli aliiweka sheria hiyo wakati wa utawala wake akiwa mfalme. Na bado hapa, anaikiuka sheria yake mwenyewe. Nini kilimbadilisha? "*Basi roho ya BWANA ilikuwa imemwacha Sauli, na roho mbaya kutoka kwa BWANA ikamsumbua*" (Samweli 16:14). Hii ilitokea baada ya Sauli kutotii amri ya Mungu ya kuwaangamiza kabisa Waamaleki (1 Samweli 15:10,11). Hata Samweli alikataa kusema naye (1 Samweli 15:35) kwa sababu ya kutotii kwake.

Mfalme Sauli alipopoteza "roho ya Bwana," hii ilileta mabadiliko makubwa ndani yake. Alipoteza roho ya akili timamu (ona 2 Timotheo 1:7) na akaanza kuamini kama mtu yeyote wa kiulimwengu. Alipokuwa hajui la kufanya, alifanya jambo lisilowazika kwa kutafuta kwanza, kisha kumtembelea mchawi. Anamhakikishia mchawi, ambaye aalikuwa na wasi wasi kwamba huenda akafa ikiwa ataendelea: "*Sauli akamwapia kwa BWANA, Hakika kama BWANA aishivyo, hutaadhibiwa kwa ajili ya jambo hili. Ndipo yule mwanamke akauliza, Nikuletee nani kwa ajili yako? Mlete Samweli, alisema. Yule mwanamke alipomwona Samweli, alilia kwa sauti kuu, akamwambia Sauli, Mbona umenidanganya? Wewe ni Sauli!*" (1 Samweli 28:10-12 ).

Inawezekana kabisa kwamba alichokiona mwanamke kilizungumza pia. Huenda kilisema kitu kama, "Amani iwe kwako, Mfalme Sauli." Kisha alitambua mara moja utambulisho wa mgeni wake na alikuwa na uhakika kwamba hii ingemaanisha kifo chake. Lakini mfalme

anajibu: “*Usiogope. Unaona nini? Yule mwanamke akasema, naona mzimu ukitoka katika nchi. Unaonekanaje? Aliuliza. Mzee aliyevaa joho anakuja, alisema. Ndipo Sauli akajua ya kuwa ni Samweli, akainama kifudifudi na kusujudu.*” (aya ya 13, 14)

Tafadhali kumbuka: **Mfalme Sauli haoni chochote hata kidogo**. Inabidi amuulize huyo mwanamke anachokiona ni nini! Anaambiwa ni mzee aliyekuwa amevaa joho. Hilo lilitosha kumfanya aamini kuwa ni Samweli. Mzuka huyo, anayezungumza kwa kutumia mwasiliani, anamwambia Sauli hivi: “*Kwa nini umenisumbua kwa kunipandisha juu? Niko katika dhiki kuu, Sauli alisema. Wafilisti wanapigana nami, na Mungu ameniacha. Hanijibu tena, ama kwa manabii au kwa ndoto. Kwa hiyo nimekuita ili uniambie cha kufanya*.” ( aya ya 15)

Katika mistari inayofuata Sauli anaambiwa kwa nini Mungu amemwacha. Mwishowe anasikia maneno haya ya maangamizi: “*BWANA atawatia Israeli pamoja na wewe mikononi mwa Wafilisti, na kesho wewe na wanao mtakuwa pamoja nami [katika hali ya kifo]. BWANA pia atalitia jeshi la Israeli mikononi mwa Wafilisti” (mstari wa 19).*

Je, “unabii” huo ulitimizwa? Israel inaingia vitani na Wafilisti siku iliyofuata: “*Basi Wafilisti wakapigana na Israel; wana wa Israeli wakakimbia mbele yao, na wengi wakauawa juu ya Mlima Gilboa. Wafilisti wakamsonga sana Sauli na wanawe, nao wakawaua wanawe Yonathani, Abinadabu na Malki-Shua. Mapigano yalikuwa makali juu ya Sauli, na wapiga mishale walipompata, wakamjeruhi vibaya sana.*” ( 1 Samweli 31:1-3 )

Sauli na baadhi ya wanawe walikufa katika vita hivyo, lakini mwana mmoja hakuwapo: “*Wakati huo huo, Abneri mwana wa Neri, mkuu wa jeshi la Sauli, alikuwa amemchukua Ish-Boshethi mwana wa Sauli na kumpeleka Mahanaimu. Akamfanya mfalme wa Gileadi, Ashuri na Yezreeli, na Efraimu, Benyamini na nchi zote Israel. Ish-Boshethi mwana wa Sauli*

*alikuwa na umri wa miaka arobaini alipoanza kutawala Israeli, akatawala miaka miwili. Hata hivyo, nyumba ya Yuda ilimfuata Daudi*." ( 2 Samweli 2:8-10 )

Ish-Boshethi mwana wa Sauli hakufa. Shukrani kwa Abneri, naye huyo Ish-Boshethi anakuwa mfalme wa makabila kumi na moja na akafa baadaye sana alipouawa (taz. 2 Samweli 4:8). Hivyo maneno yaliyotamkwa kwa Sauli kupitia mwaguzi yalitimia kwa kama 80% (Sauli na wanawe watatu kati ya wanne walikufa siku iliyofuata). Unabii wowote uliotolewa na nabii Samweli alipokuwa hai siku zote ulitimia kwa 100%.

Kwa hiyo ni nani huyu "Samweli" ambaye Sauli anafikiri anazungumza naye? Si mwingine bali ni "baba wa uongo," Shetani, akijifanya kuwa nabii Samweli. Ili kueneza uongo wake wa kwanza (taz. Mwanzo 3:4) anaiga wafu ili kutoa hisia kwamba kuna maisha baada ya kifo. Kupitia njia ya mwaguzi anajifanya kuwa nabii Samweli na kufanya utabiri. Alijua mengi kuhusu hali ya Mfalme Sauli na vita ambavyo vingepiganwa na Wafilisti siku iliyofuata. Siku hizo wafalme waliongoza majeshi yao wakipigana na mfalme wa jeshi pinzani. Wana wa mfalme walikuwa pamoja naye kwa ujumla. Hivyo mfalme aliyepoteza mara kwa mara angepoteza maisha yake au kujeruhiwa vibaya sana, pamoja na wanawe. Hakukuwa na swali kwamba Mungu alikuwa amemwacha Sauli, vinginevyo Sauli hangetafuta ushauri kwa mchawi(mwaguzi). Kwa hiyo akiwa na hili akilini Shetani alikisia jinsi matukio ya wakati ujao yangetokea. Lakini kubahatisha bado ni kubahatisha tu na huwa sio sahihi kwa 100%.

Kwa maelfu ya miaka Shetani amewadanganya watu kupitia wawasiliani wa kiroho na waaguzi kwa kudai kwamba ana uwezo wa kutoa unabii kuhusu wakati ujao. Anapata uaminifu kwa kuelezea kwa usahihi siku za nyuma na kisha, kulingana na taarifa zote

alizonazo, hufanya ubashiri kuhusu siku zijazo ambapo mafanikio hayawezi kuwa 100%. Mungu pekee ndiye anayejua wakati ujao (taz. Isaya 46:10 na 42:9).

**Yesu Kubadilika Sura**

Karibu na mwisho wa maisha yake, Yesu alifanya tukio ambalo lilishuhudiwa na wafuasi wake watatu: *"Baada ya siku sita Yesu akawachukua Petro, Yakobo na Yohana nduguye Yakobo, akawaleta juu ya mlima mrefu peke yao. Huko aligeuka sura mbele yao. Uso wake ukang'aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru. Wakati huo Musa na Eliya wakatokea mbele yao, wakizungumza na Yesu."* ( Mathayo 17:1-3 )

Petro, Yakobo, na Yohana walijuaje ni nani aliyekuwa pamoja na Yesu? Bila shaka ni kwa sababu walisikia walichokuwa wakizungumza. Katika kipindi cha mazungumzo Yesu pengine alitumia majina yao alipokuwa akizungumza nao. Lakini swali la msingi zaidi ni jinsi gani manabii wawili waliokufa wangeweza kuzungumza na mtu yeyote. Je, "nafsi" zao zilikuwa hai na ziliweza kuzungumza? Ikiwa ndivyo, inapingana na fundisho la Biblia la nafsi kufa na kwamba hakuna uhai baada ya kifo.

Jambo moja ni muhimu sana kuhusu tukio hili: "*Na walipokuwa wakishuka mlimani, Yesu akawaonya, akisema, Msimwambie mtu ye yote habari ya **maono hayo**, hata Mwana wa Adamu atakapofufuka katika wafu*" (Mathayo 17:9 KJV) Watatu hao walikuwa wameona "maono" sawa na maono yaliyorekodiwa kibiblia katika Kitabu cha Ufunuo, au maono ya mtume Paulo katika 2 Wakorintho 12:1-4, au maono ya mtume Petro katika Matendo 10:10-16. "Maono" sio uhalisia. Ni taswira inayofanana na tunayoiona ndani ya nyumba zetu kupitia televisheni. Katika vipindi vya televisheni watu waliokufa wanaonekana wakitembea na kuzungumza. Kila mtu anajua kuwa hawako hai kwa sababu ni yale ni "maono" tu.

Maono haya kubadilika sura yalikuwa uwakilishi wa picha wa ufalme wa Mungu utakaokuja duniani chini ya utawala wa "Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana." Musa aliwakilisha sehemu **inayoonekana** ya ufalme huo, sehemu ya kimwili, itakayokuwa na Mababu wa Imani, wale waliokuwa waaminifu kwa Mungu kabla ya Yesu. Eliya aliwakilisha sehemu **isiyoonekana** ya ufalme huo, sehemu ya kiroho, inayojumuisha Yesu Kristo pamoja na Kanisa lake, wafuasi wake waaminifu waliojitolea maisha yao kumfuata. Yesu anatawala na kuratibu sehemu(pande) zote mbili kama inavyoonyeshwa katika "Musa na Eliya wakizungumza naye." Hii ilikuwa taswira inayoonekana ya utukufu ujao wa Yesu katika ufalme wake.

**Mwizi Msalabani**

Muda mfupi tu kabla ya kufa kwake, Yesu alimgeukia mwizi aliyekuwa akining'inia kwenye msalaba karibu naye na kusema: "*Nakuambia kweli, leo utakuwa pamoja nami katika paradiso*" (Luka 23:43). Mwizi huyu alikuwa ameomba radhi kwa Yesu na, kama wengi wanavyoelewa maneno haya, aliambiwa kwamba angeenda mbinguni siku iyo hiyo. Lakini mwizi hakuomba kitu kama hicho. Hiki ndicho alichouliza: "***Unikumbuke** utakapoingia katika ufalme wako*" (Luka 23:42). Aliomba nafasi ya kibali katika ufalme wa Yesu, na wala si kwenda mbinguni. Hata wafuasi wa karibu wa Yesu hawakuuliza jambo kama hilo la kwenda mbinguni. Hawakuwa na shauku ya kwenda mbinguni. Walikuwa wakitafuta kitu tofauti kabisa. Baada ya kifo na ufufuo wake, waliuliza: "*Bwana, wakati huu utaurudisha ufalme tena Israel?*" (Matendo 1:6) Walitazamia kuwa sehemu ya ufalme wa kidunia wa Israeli ambao ungekwezwa kati ya mataifa mengine ya ulimwengu. Mara nyingi walibishana wenyewe kwa wenyewe kuhusu ni nani angepokea heshima kubwa zaidi katika ufalme huo: "*Kukatokea mzozo kati yao kuhusu ni nani kati yao anayehesabiwa kuwa mkuu zaidi*" (Luka 22:24). Wanafunzi hawakuweza kuelewa mbingu

wala hawakuwa na shauku yoyote ya kimbingu hadi walipopokea roho takatifu siku ya Pentekoste.

Wakati wezi wawili waliposulubishwa, awali walimtukana Yesu pamoja na umati wa watu waliokuwa wakitazama (taz. Mathayo 27:44 na Marko 15:32). Lakini baadaye sana baada ya kumtazama Yesu, mmoja wao alitambua kwamba Yesu hakuwa na hatia: "*Mmoja wa wale wahalifu waliotundikwa hapo alimtukana: Je, wewe si Kristo? Jiokoe mwenyewe na sisi! Lakini yule mhalifu mwingine akamkemea. Akamwambia je, hamwogopi Mungu, kwa kuwa uko chini ya hukumu iyo hiyo? Tunaadhibiwa kwa haki, kwani tunapata yale yanayostahiki matendo yetu. Lakini mtu huyu hakutenda kosa lolote.*" (Luka 23:39-41 )

Juu ya kichwa cha Yesu kulikuwa na ubao: "*Kulikuwa na maandishi juu yake, yaliyosomeka: HUYU NDIYE MFALME WA WAYAHUDI* " (Luka 23:38). Leo tunaona mara kwa mara herufi INRI kwenye ubao mdogo kwenye misalaba. Hizi ni herufi za kilatini. Katika Kilatini herufi hizo zina maana hizi: I = Isus (Yesu), N = Nazarainus (wa Nazareti), R = Rex (Mfalme), I = Idurum (wa Wayahudi). Alipouona ubao huo juu ya kichwa cha Yesu, mwizi huyo alipata msukumo wa kuomba jambo kwa Yesu ambaye angeweza kuwa mfalme mwenye ufalme. Hakika hakuwa na la kupoteza kwa kuuliza.

Mwizi huyo aliungana na Yesu "siku ile," lakini haikuwa katika "paradiso." Siku hamsini baadaye, siku ya Pentekoste, Petro alizungumza na umati na kusema: [Daudi] "alisema juu ya ufufuo wa Kristo, ya kwamba nafsi yake **haikuachwa kuzimu**, wala mwili wake haukuona uharibifu" (Matendo 2:31, *KJV* ). Yesu alikuwa katika "kuzimu" kwa siku tatu hadi ufufuo wake!

Uwekaji wa alama ya mkato katika maneno ya Luka 23:43 unaleta tofauti kubwa: "Nakuambia kweli, leo utakuwa pamoja nami peponi [wakati fulani katika saa chache zijazo]" dhidi ya "Nakuambia kweli

leo, utakuwa pamoja nami katika paradiso [wakati fulani katika wakati ujao usiojulikana].” Alama ya mkato inapaswa kuwa mbele ya neno **leo** na sio mbele ya neno **kweli**. Paradiso, bila shaka, inahusu ufalme wa Kristo ujao. Lakini ufalme huu haukuanzishwa miaka elfu mbili iliyopita, na bado haujaanzishwa. Bwana alimhakikishia mwizi kwamba ufalme wake utakapokuja, mwizi atapokea baraka alizoomba. Isipokuwa kwa ahadi hii kutoka kwa Yesu mwizi hakupata baraka siku hiyo.

Maandishi ya asili ya Kiyunani ya Agano Jipya yaliandikwa kwa herufi kubwa na hayakuwa na alama za uakifishaji na hakuna nafasi kati ya maneno. Migawanyiko ya sura ilibuniwa na Stephen Langton, Askofu Mkuu wa Canterbury, Uingereza mwaka 1227 BK. Mgawanyo wa sura katika mistari ulifanywa na Robert Estienne mwaka wa 1551. Mfumo wake ulitumiwa katika Biblia ya Geneva mwaka 1560 na karibu matoleo yote ya Biblia tangu hapo. Alama za uakifishaji zilikuja baadaye. Ingawa alama za uakifishaji kwa ujumla ni baraka kubwa kusaidia kuelewa, hili ni tukio moja lilipofanywa isivyofaa na kutoa maana yasiyofaa.

Mwizi alikufa na bado amekufa. Atafufuka siku ya ufufuo na ataheshimishwa ipasavyo wakati ambapo “kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri” (Warumi 14:11). Maneno ya fadhila ya mwizi kwa Bwana pale msalabani yatamfanya “akumbukwe” katika utukufu wa ufalme wa Yesu duniani.

### Kuhifadhiwa Roho na Nafsi Yenu Yote

Mtume Paulo aliandika hivi: *“... Nanyi mhifadhiwe roho yenu na* ***nafsi*** *yenu na mwili wenu wote, bila lawama, hata wakati wa kuja kwake Bwana*

*wetu Yesu Kristo*" (1 Wathesalonike 5:23[2]). Wengine wanadhani hii ina maana kila mwanadamu ana nafsi na mwili na roho tofauti, lakini hiyo si kweli. Kulikuwa na washiriki wengi wa kanisa la Thesalonike, lakini Paulo anazungumza juu ya roho moja, nafsi moja, na mwili mmoja.

Paulo alianza kwa maneno haya: "*Paulo, Sila na Timotheo, kwa kanisa la Wathesalonike, katika Mungu Baba, na katika Bwana Yesu Kristo: Neema na amani iwe kwenu*" (1 Wathesalonike 1:1). Anaelekeza barua hiyo si kwa watu binafsi bali kwa kanisa kwa ujumla. Kama ingeelekezwa kwa watu binafsi, angaliandika, "Roho zenu na nafsi zenu **na miili** yenu **ihifadhiwe** bila lawama" (ambavyo ndivyo ilivyoandikwa kimakosa katika Biblia nyingi za Kiswahili)

Lakini je, kanisa lenye washiriki wengi linawezaje kuwa na roho moja na mwili mmoja na nafsi moja? Katika barua nyingine Paulo aliandika hivi: "*Fanyeni bidii kuuhifadhi umoja wa Roho kwa kifungo cha amani. Kuna mwili mmoja na Roho mmoja, kama vile mlivyoitiwa tumaini moja mlipoitwa.*" (Waefeso 4:3,4) Kwa Paulo kanisa ni kitu kimoja chenye mwili mmoja na roho moja.


Mapema katika historia ya kanisa tunaambiwa hivi: "*Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na nafsi moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu cho chote alicho nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika.*" (Matendo 4:32, *KJV* ). Kanisa, kwa pamoja, linaelezewa kuwa ni chombo kimoja, kilicho hai. Hii ni sawa sawa na jinsi mtume Paulo alivyolitaja kanisa katika barua yake kwa Wathesalonike.

---

[2] Tafsiri nyingi za Biblia za Kiswahili zimetumia maneno "nafsi zenu na roho zenu na miili yenu" kana kwamba ni katika uwingi, lakini hii ipo kimakosa kwa sababu toleo la asili halijatumia uwingi bali umoja nalo ndilo sahihi.

Fundisho la Biblia kuhusu kifo cha nafsi linapatana kikamilifu katika Agano la Kale na Agano Jipya. Neno "nafsi" daima hurejelea kiumbe hai chenye mwili na pumzi ya uhai. Haya kwa pamoja hutokeza nafsi ambayo ina uhai, akili na moyo. Upinzani mwingine pekee unaoonekana ni fumbo/mfano wa Yesu kuhusu **Tajiri na Lazaro** katika Luka 16. Ni muhimu vya kutosha kwamba tutatoa somo letu linalofuata kwa hilo (kujadili utata huo).

**-Amina-**



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***